**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**KIDATO CHA TATU**

**MUDA: SAA $2^1/2$**

**NOVEMBER 2021**

**MAAGIZO:**

- **Jibu maswali MATATU pekee**
- **Swali la KWANZA ni la LAZIMA**
- **Maswali mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki**
- **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja**
- **Kila swali lina alama ishirini**

SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

**<u>1.SEHEMU YA D: USHAIRI</u>**

Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa
Kalia kinaya, dagaa, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa

Na sio mzigo, kijana, bado wafaa
Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa
Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, ndani hukaa,
Kuliko vigogo, dagaa, hajambaa
Hapati kipigo, dagaa, hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa
Sihofu magego, kijana, nawe wafaa
Kazana kidogo, kijana, kugaaga

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 1)
(b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili (alama 4)
(c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake (alama 3)
(d) Tambua bahari katika shairi hili (alama 3)
(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi (alama 3)
(g) Eleza toni la shairi hili (alama 2)

## FASIHI SIMULIZI

2i) Eleza umuhimu wa Ngano za mtanziko katika jamii (al.5)

(ii) Fafanua umuhimu wa maigizo ya watoto (al.5)

(iii) Sifa tano za rara (al.5)

(iv) Eleza dhima ya misimu kama kipera cha usemi (al.5)

3. [a ]Maigizo ni nini? ( al.2)

[b] Fafanua sifa nne za maigizo. Al.4)

[c] Eleza vikwazo vya ukuwaji wa fasihi simulizi. Al.10)

[d] eleza tofauti kati ya misemo na misimu. Al.4)

TAMTHILIA YA KIGOGO (PAULINE KEA)

4.`…………….wanadai kitu kikumbwa au kitu chote!`

a)Eleza muktadha wa dondoo hili al 4

b)Tambua maudhui yanayodokezwa kwenye dondoo hili al 2

c)Kwa kutumia hoja sita eleza namna maudhui uliotaja hapo juu yanavyojitokeza katika tamthilia ya kigogo al 6

d)Fafanua sifa za msemewa al 4

e)fafanua umuhimu wa msemaji al 4

5: Jadili jinsi dhuluma inavyojitokeza katika Tamthilia ya Kigogo. **(al 20)**

**CHOZI LA HERI- A. MATEI**

6.“Mbona huna bashasha za kijana wa umri wako.”

a) Eleza muktadha wa maneno haya. la 4)

b)Ni yapi yalifuata baada ya maneno haya. ala 12)

c)Eleza sifa nne za msemewa ala 4)

7.“Riwaya ya Chozi la Heri inaakisi uozo uliomo katika Jamii nyingi barani Afrika”

Thibitisha kauli hii kwa kurenjerea Riwaya al20